# 6 Uvuvi

*Ni Yeye (Mwenyezi Mungu) aliyekudhalilishieni bahari mkala kutokana nayo samaki safi na mkatoa kutokana nayo mapambo mnayoyavaa na mkaviona vyombo vya baharini vikipita juu yake ili kutafuta fadhila zake ili mpate kushukuru. (Qur'an 16:14)*

## Uvuvi ni nini?

Neno uvuvi hutumika kumaanisha harakati au kitendo cha kuvua samaki katika eneo maalum. Uvuvi hujumuisha uvuaji wa samaki kutoka maeneo ya bahari, maziwa au mito au katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ufiugaji wa samaki. Ama kwa Zanzibar uvuvi hufanyika kwa maeneo ya baharini zaidi. Uvuvi hugawanywa kulingana na aina ya samaki wanaovuliwa, aina ya njia za uvuvi zinazotumika pamoja na mitego, vyombo na pia maeneo ambayo uvuvi hufanyika. Baadhi ya wavuvi huwatumia samaki kwa ajili ya kujikimu, baadhi kwa ajili ya biashara na baadhi kwa ajili ya kujifurahisha.

## Ni aina ngapi za uvuvi zinazofanyika Zanzibar?



**Uvuvi asilia aina ya dema © Nell Hamilton**

Ziko njia nyingi za uvuvi zinazofanyika Zanzibar. Wavuvi hutafuta aina mbali mbali za samaki katika maeneo tofauti kwa kutumia mbinu mbali mbali. Wavuvi wengi wa Zanzibar ni wavuvi wadogo wadogo, ambao ambao huendesha shughuli zao katika maeneo ya matumbawe ambayo yapo katika maeneo ya mwambao ambapo usafiri wa kijadi kama vile ngalawa, dau, mitummbwi, mashua vina uwezo wa kufika. Pia mitego ya aina mbalimbali hutumika kama vile madema, uzio, jarife, mishipi n.k. vile vile kuna utamaduni wa kuokota kombe na chaza na wanyama wadogo wadogo wa baharini katika maeneo ya fukwe yanayotokewa na maji. Hili ni maarufu miongoni mwa wanawake na watoto ambao hutumia mazao wayapatayo kwa kujikimu na hata kwa biashara.

Wakati samaki wengi wanaopatikana hutumika kwa kujikimu (chakula) au kuuzwa katika soko la ndani, mahitaji ya samaki yanaongezeka kwani hoteli na migahawa mingi ya kitalii inahitaji samaki wa aina ya hadhi ya juu kama vile ngisi, pweza, kaa, nduaro na nguru. Hivi sasa wawekezaji kutoka nje wanajaribu kuikuza na kuipa uwezo sekta ya uvuvi. Mashua, ngalawa za mashine zinawawezesha wavuvi kwenda mbali zaidi kutafuta samaki, pia nyavu kubwa zinatumika kukamata samaki zaidi ukilinganisha na mbinu za kizamani. Mbinu hizi zinawawezesha wavuvi wa Zanzibar kuwafikia hata wavuvi wa Tanzania Bara. Matumizi ya njia zisizofaa na zisizokubalika kisheria kama vile makorokoro, mishale, bunduki ya majini, sumu, mripuko / baruti, nyavu za kukokota na beach seines umeongezeka pia.

Uvuvi wa burudani 'game fishing' bado haujaenea kwa kiasi kikubwa katika Zanzibar, lakini unaonekana kupata umaarufu kwa watalii. Uvuvi wa samaki kama burudani kwa kawaida hufanyika kwa kutumia boti maalumu kwa kutumia ujiti na mishipi ambayo hukusudia kukamata samaki wa aina mbali mbali kuu kama vile nduwaro, samsuli papa. Kwa Zanzibar, samaki wa aina hizi hutafutwa na wazamiaji hasa watalii ambao hutumia bunduki ili kuwapata hii ni njia haramu hapa.

## Kwa nini uvuvi ni muhimu Zanzibar?

Jamii zinazoishi katika maeneo ya mwambao kote Zanzibar wanategemea kwa kiasi kikubwa rasilimali za bahari kwa maisha yao. Watu wengi huishi maisha ya kimila ikiwa ni pamoja na kujitafutia chakula kwa mujibu wa mahitaji. Samaki huwapatia asilimia 98 ya protini wa wale waishio kwa mlo wa kipato cha chini hapa Zanzibar. Kwa familia nyingi samaki hutumika kama ni njia kuu ya kujipatia kipato pia. Takriban wavuvi wapatao 34,000 wanajiajiri katika sekta hii. Kwa kawaida samaki wanaopatikana huuzwa katika soko la ndani. Karibu tani 24,000 za samaki hupatikana kwa mwaka wenye thamani ya shilingi 36 milioni kwa uchumi wa Zanzibar.

Uvuvi pia una umuhimu katika masuala ya utamaduni kwani familia za wavuvi zimeanza vizazi vingi nyuma. Hivyo ni muhimu sana kwa jamii zinazoishi maeneo ya mwambao. Pia inatoa ajira kwa wauzaji na watengenezaji vyombo vya kuvulia na mitego ya kuvulia pia.

Kiasi kikubwa cha utalii wa Zanzibar unaendeshwa kwa kutumia hadhi yake kimataifa ya viumbe wa baharini, kwani watalii wengi huvutika na vyakula vizuri vitokanavyo na mazao ya baharini, michezo ya baharini (kufuta pumzi baharini) na kuzamia kuangalia samaki wa aina mbali mbali wenye rangi za kupendeza, bustani za miamba na mamalia wanaopatikana baharini. Jambo hili huleta ajira nyingi katika Zanzibar ambazo pia zinategemea kuendelea kuwepo kwa rasilimali hai katika maeneo ya mwambao.

## Ulikua unajua...?

- Wavuvi kusini ya Unguja walitumia nyama ya pomboo kama chambo cha kuvulia papa. Hii ni kwa sababu nyama yake ina damu nyingi ambayo huwavutia papa. Lakini sasa wananufaika mno kupitia utalii wa pomboo, sasa hawavui tena pomboo!
- Pono wanaweza kuzalisha mchanga. Wanauchukua kutoka kwenye miamba na kuutoa kupitia tundu za choo kama udongo. Samaki mmoja ana uwezo wa kutengeneza kilo 90 za mchanga kwa mwaka!
- 'Reef balls' (vitufe vya matumbawe) ni vitufe vya kutengenezwa ambavyo viliwekwa baharini na kufanya makazi ya matumbawe na yanatumika kuhifadhi matumbawe Pemba kote!
- Bioanuwai vinaopatikana katika kisiwa cha Chumbe ni wengi zaidi kuliko wanaopatikana nje ya kisiwa hicho. Kaika $km^2$ 0.4 za hifadhi mna miamba 200 na spishi 400 za samaki.
- Pia samaki wapatikanao ndani ya hifadhi ya kisiwa cha Chumbe ni wakubwa zaidi na wengi kuliko maeneo mengine ya nje ya kisiwa, kiwango cha samaki kwa kilomita za mraba kinakisiwa kuwa mara tatu zaidi ya samaki wanaopatikana maeneo ya nje ya kisiwa!

## Nini athari zinazokabili uvuvi?

***kuvua kupita kiasi –*** Mvuvi yeyote ukimuuliza anaweza kukwambia kwamba hakuna samaki wengi sasa kama ilivyokuwa hapo kabla, na wanalazimika kusafiri mbali zaidi kuliko walivyokuwa wanafanya kupata kiwango kile kile cha samaki. Kuna sababu nyingi zinazopelekea hali hii zikiwemo hizi zifuatazo: kuongezeka kwa idadi ya wavuvi, kuongezeka kwa vyombo vya uvuvi ambavyo ni vikubwa na wavuvi wanatumia nyavu kubwa zaidi kama vile jarife nyavu kubwa na ushashi zenye macho madogo zaidi, ukilinganisha na zamani. Maji ya Zanzibar pia yanawavutia wavuvi kutoka maeneo mengine (wavuvi wahamiaji) au kwa jina maarufu kama ujulikanavyo uvuvi wa 'dago' kwa sababu samaki wa maeneo yakaribu yameshaharibiwa mno. Baya zaidi hadi sasa ni kutumika kwa jarife ndefu zenye urefu wa karibu mita 900 ambazo hutegwa katika bahari yenye kina kirefu ili kukamata samaki kama vile nguru, nduwaro, tuna na samsuli. Pia kuwepo kwa nyavu zinazotegwa chini zenye urefu wa hadi mita 450 ambazo hutegwa karibu sana na maeneo ya fukwe ili kukamata samaki kama vile papa na vinyenga au taa.

Mwanzoni mwa utumiaji wa mbinu hizi samaki wengi walipatikana hivyo, idadi ikapungua. Aina chache tu za samaki wanazaa haraka, na idadi yao ingeweza kurejea haraka baada ya shindikizo kubwa la Uvuvi linaposita, lakini wengi wao wakiwemo papa na chewa huzaa kwa taratibu sana na yawezekana wasiweze kurejea katika hali yao ua awali. Hivyo basi ni muhimu kufahamu ikolojia ya ya samaki ambao tunawategemea na kufuatilia taathira zinazokana na uvuvi kwa ukaribu zaidi. Wanasayansi wanaofuatilia uwepo wa samaki wamethibitisha kile ambacho wavuvi wanakijua: samaki wapatikanao katika maeneo ya ndani ya mwambao wa Zanzibar ambao tunakula wanazidi kuwa wadogo na wanazidi kupungua kila mwaka. Kama hili halikuzuiwa basi baadae tutakuwa hatuna samaki watakaobaki kabisa!

***Mbinu za uvuvi zisizofaa? –*** Pamoja na kwamba samaki hupatikana wengi zaidi ukilinganisah na zile mbinu za kizamani, mbinu mpya za uvuvi zina onekana kuharibu zaidi makazi ya samaki. Nyavu za kukokota huyavunja na kuyaharibu matumbawe, na wavuvi wa makokoro na wavuvi wa baruti huyang'oa matumbawe na kuyaacha vipande vipande hali ambayo hupelekea kuuwa kila kitu, vinavyoliwa na visivyoliwa. Miamba ya matumbawe na vitalu vya nyasi bahari yanayoharibiwa kwa njia hizi za uvuvi huchukua miaka mingi kurejea katika hali yake ya awali. Hivyyo njia zote hizi zimepigwa marufuku katika bahari ya Zanzibar, hata hivyo ni vigumu kufuatilia kufanya doria katika bahari kuu na vitendo hivi bado haramu viaendelea katika baadhi ya maeneo.

***Kukamata samaki bila kukusudia –*** Hii ni njia ambayo samaki hukamatwa kwa bahati mbaya katika mitego iliyowekwa kukamata samaki wa aina fulani. Kwa kawaida katika baadhi ya nchi, samaki wapatikanao kwa njia hii huwa hawahitajiki hivyo hutupwa wakiwa wafu hivyo hakuna anaenufaika, lakini Zanzibar kila kitu kinaliwa. Baadhi ya mbinu za uvuvi kama vile madema huwakamata samaki wachache wa aina hii, lakini baadhi ya mitego kama vile wavu wa kukokota, jarife na nyavu za kutega chini ya maji hukamata samaki wengi zaidi wasiowataka kuliko wale wawatakao. Walio katika hatari zaidi hususan kwa nyavu kubwa ni viumbe wapatikanao baharini kama vile nyangumi, pomboo, nguva na kasa. Matukio mengi ya kukamatwa kwa viumbe vya baharini hapa Unguja hutokea katika nyavu zinazotegwa katika maeneo ya Kaskazini ya kisiwa cha Unguja na idadi kubwa ya pomboo na aina mbali mbali za kasa zinaendelea kupungua.



**Kasa walio hatarini sana kutoweka akiwa amekamatwa na kuuwawa katika nyavu iliyotelekezwa visiwani Zanzibar © Nell Hamilton**

***Nyavu zilizotelekezwa*** **–** Iwapo mvuvi atapoteza madema kwa sababu ya kuharibika au kupotea kwa boya, basi mtego ambao umetengenezwa kwa nyenzo za kimaumbile, taratibu nyenzo hizo huanza kuteketea. Lakini cha kusikitisha ni kwamba nyavu za kisasa zimetengenezwa kwa kutumia nyenzo ambazo haziwezi kuvunjika au kuoza, hivyo ikiwa zitapotea zitaendelea kukamata na kuua viumbe wa baharini kwa karne nyingi.

***Uchafuzi wa mazingira*** **–** Athari za uchafuzi wa mazingira katika uvuvi zinaweza kuwa mbaya sana. Samaki wanaweza kukutana na vipande vya plastiki wakavila. Vipande hivi vya plastiki huziba matumbo yao na hufa kwa njaa. Maji machafu yasiyotiwa dawa yanaweza kuchafua vyakula vya baharini vipatikanavyo katika maeneo ya fukwe ambapo vikitumiwa vinaweza kusambaza maradhi yanayouwa kama vile kipindupindu na homa ya matumbo. Kemikali za sumu zipatikanazo kwenye madebe ya takataka, wakulima wanaotumia mbolea za kemikali na madawa ya kuulia wadudu, zinazoingia baharini ambazo hujijenga katika tishu za viumbe wa baharini wanavyovila, hivi vinaweza kusababisha ugumba, kensa, na maradhi mengine kwa samaki na binaadamu, na pia vinaweza kusababisha vifo. Kiwango cha sumu huongezeka kila mfuatano wa chakula unavyopanda, hivyo kuendelea kuleta madhara kwa watu wanaotumia samaki waliobeba vimelea, watoto ndio hasa walio katika hatari zaidi.



**Watoto hukusanya samaki wa magamba katika pwani ya Zanzibar © Nell Hamilton**

## Vipi tunaweza kulinda uvuvi wa Zanzibar?

Zanzibar si nchi ya mwanzo kukutwa na changamoto kama hizi, na ziko njia nyingi za utatuzi ambazo zimetumika kwa mafanikio katika maeneo mengine. Iwapo watoto au watu wazima, mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu, tunaweza kusaidia kulinda Uvuvi wetu na kuhifadhi uwezo wa kuishi kwa vizazi vijavyo.

***Maeneo ya hifadhi ya bahari (MPAs)*** **–** Kama ilivyo kwa matumbawe, njia moja nzuri zaidi ya kutunza mazalio ya samaki ni kuanzisha maeneo ya hifadhi ya baharini, maeneo ambayo shughuli za uvuvi zitapigwa marufuku. Maeneo haya huhifadhi matumbawe, mikoko na nyasi bahari ili yasiharibiwe: hii itasaidia kuhifadhi maeneo ambayo samaki watazaliana na itakuwa ni kama vitalu kwa samaki wadogo kuweza kukua. Watatoa chakula kwa aina nyengine za samaki, na itakuwa ni eneo la hifadhi kwa aina nyengine za samaki ambazo ziko hatarini kutoweka. Katika baadhi ya maeneo ya hifadhi, uvuvi hupigwa marufuku, wengine huruhusu ili watu wavue kujikimu tu na sio kwa kutumia njia zisizofaa za uvuvi. Kwa kawaida maeneo haya huwa katikati ya maeneo ambayo uvuvi unaruhusiwa. Uvuvi huzuiliwa kwa baadhi ya nyakati ili kudhibiti aina fulani ya samaki wakati wa kuzaliana kwao lakini watu huruhusiwa kuvua bada ya muda fulani. Kwa hivi sasa hapa Tanzania asasi nyingi za kiraia zimeanzishwa na vikundi vya wavuvi ili kuwawezesha kupata samaki wa kutosha sasa na kuhifadhi mazalio ya samaki kwa ajili ya baadae.

Ingawa uvuvi huzuiliwa katika maeneo ya hifadhi, kwa ujumla wanaonufaika ni wavuvi. Huwapa samaki hifadhi na chakula cha kutosha ambapo hukua kwa ukubwa wa kuridhisha bila ya kuvuliwa. Huzaliana vizuri na hukua kwa haraka, na huzaliana kwa wingi na hukuza hifadhi. Baada ya kukuwa vizuri baadhi ya samaki huhamishiwa katika maeneo ya karibu na hifadhi ambapo uvuvi huruhusiwa. Hivyo samaki wapatikanao maeneo ya karibu na hifadhi huwa ni wakubwa zaidi na ni wengi kuliko wanaopatikana mbali na maeneo hayo. Hali hii hujitokeza karibu mita 500 kutoka eneo la hifadhi na ni eneo maarufu sana kwa wavuvi. Na hii ndio maana wavuvi wengi huvua nje kidogo ya eneo la hifadhi katika kisiwa cha Chumbe. Hii ni kwa sababu wanajua watapata samaki zaidi kuliko watakapovua maeneo mengine na pia watapata pesa zaidi. Bila shaka maeneo ya hifadhi yanahitaji kuchungwa sana ili kuhakikisha kwamba sheria zinafuatwa na jamii zinanufaika kutokana na maeneo ya hufadhi. Hivyo basi hili litafanyika zaidi iwapo kutakuwa na mfumo wa kuishirikisha jamii katika utekelezaji. Mpango wa udhibiti wa maeneo ya pwani lazima uhakikishe kwamba matumbawe, majani ya pwani na mikoko vyote vinahifadhiwa. Kanuni zilizowekwa kulinda bidhaa ya samaki lazima zitumike na kufanyiwa kazi ipasavyo.

***Kusaidia mfumo wa uvuvi endelevu*** **–** Wavuvi wanaweza kusaidia uvuvi uwe na faida kwa kutumia mbinu endelevu na pia kusaidia kuwaelimisha wenzao kufanya hivyo. Kwa mfano:

- Acha kukamata makundi adimu ambao hawazaliani kwa haraka, kama vile papa, taa vinyenga, nduwaro na samaki ambao ni muhimu kiikolojia kama vile pono, kikande na tritoni.
- Tumia nyavu zenye macho makubwa ili kuepuka kukamata samaki wachanga.
- Epuka kuharibu matumbawe kwa kutumia nanga, boti, nyavu, na mitego mengine au hata kutembea tembea juu yake.

### Tembea ujionee!

- Tembelea bandari ya samaki kama Malindi au Mkokotoni – au ufukwe ulio karibu.
- Tembelea masoko ya samaki ya Chwaka, Matemwe, Uroa, Darajani, Nungwi au Pwani Mchangani.
- Ongea na wavuvi katika familia yako na jamii kuhusu jinsi mitego na njia za uvuvi zilizobadilika.

- Kamwe usivue samaki ambao wako katika hatua ya kuzaliana.
- Tumia mbinu bora za uvuvi ili kuepuka kukamata samaki usiowahitaji hususan mamalia (pomboo, nguva na nyangumi) wa baharini na kasa.
- Hakikisha kwamba mitego yako haipotei kirahisi baharini.
- Heshimu maeneo ya hifadhi yaliyopo na ungana na wavuvi na wanajamii wengine kuanzisha maeneo ya hifadhi au maeneo tengefu ili kulinda mazalio ya samaki kwa ajili ya baadae.




**Mkulima wa mwani Zanzibar © Nila Uthayakumar**

***Maisha mbadala –*** Kwa kadri idadi ya watu inavyoongezeka hapa Zanzibar, watu wanahitaji njia endelevu ili waishi bila kuharibu mazalio ya samaki yanayoteketea. Katika kulifanikisha hili mambo mengi yanaendelea kujitokeza:

*Kwanza, kilimo cha mwani:* Kilimo hiki kimeeenea takriban maeneo mengi ya Zanzibar ambapo asilimia kubwa ya wakulima wa mwani ni wanawake ambao huotesha mwani kwa kutumia kamba na vijiti katika maeneo ambayo maji hupwa na kujaa kwa ajili ya kusafirisha nje. Hii ni njia moja muhimu ya kujitafutia maisha ambayo huzalisha zaidi ya tani 7000 kwa mwaka.

*Pili, ufugaji kaa:* Baadhi ya jamii huwakusanya kaa wadogowadogo na kuwaweka katika eneo la mikoko na kuwazunguushia nyavu au vijiti ili kuwalinda na maadui zao. Humo kaa hupewa chakula chenye wanga wa kutosha hivyo hufikia kiwango cha kuuzwa kwa haraka.



**Lulu za Fumba © Narriman Jiddawi**

*Ukulima wa lulu:* Wanajamii wengi katika Ghuba ya Fumba hulima lulu kwa kutumia chaza wanaowapata katika maeneo yao ikiwa ni njia moja ya kujipatia kipato. Soko kwa ajili ya lulu zinazozalishwa Zanzibar linapatikana kupitia maelfu ya watalii wanaotembelea Zanzibar kila mwaka, lakini ni muhimu kuhakikisha ya kuwa chaza wanaendelea kuwepo. Ili kutekeleza hili vijiji vinavyofanya shughuli hii hapa Zanzibar vimeanzisha maneo tengefu.

*Utalii endelevu:* Njia muhimu sana ambayo maeneo ya hifadhi huongeza pato la kaya ni kwa kuzalisha ajira mpya. Kwa kupitia watu kama vile; msimamizi wa maeneo ya hifadhi, manahodha wa boti, wana mgambo, waongozaji katika masuala ya kupiga mbizi, wahudumu wa hoteli na waongozaji katika masuala ya kuvua. Mbali na hayo, watalii hutupatia soko kwa kazi za mikoko zinazotengenezwa kwa kutumia maligahafi za ndani.

*Uvuvi wa burudani:* Huu uvuvi kwa njia ya michezo amba baada ya kupigwa picha samaki waliokamatwa huachiwa wakiwa hai na hurejeshwa baharini.

***Matendo ya watumiaji –*** Ili kuunusuru uvuvi lazima sote tufanye kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba uvuvi unafanyika katika utaratibu endelevu ili watu waweze kujipatia mahitaji yao kutokana na rasilimali za kimaumbile na waweze kusaidia familia zao kwa sasa na pia vizazi vijavyo. Ikiwa kila mmoja ataonesha mwamko katika jamii yake na kuwasaidia wavuvi ambao wanavua samaki kwa njia endelevu, basi makundi ya samaki adimu yangebaki na samaki wa kutosha wangeendelea kuzaliana. Hebu tujenge kawaida ya kuuliza ni vipi samaki wamepatikana, na tuache kununua samaki adimu, wadogo, au samaki waliopatikana kwa kutumia mitego iliyopigwa marufuku mitego ambayo huwafanya watu wa kawaida wakose shughuli ya kufanya na kuhatarisha vizazi vijavyo kukosa kabisa kutumia samaki watokanao na mazingira yao. Hasa katika maeneo ya mikahawa tutoe mwamko kwa wafanyakazi na tubuni mbinu mbadala za kuwafanya samaki waliomo hatarini kutoweka wasiingie katika orodha ya vyakula mahotelini na baharini.

### Kitunze kidumu!

- Saidia katika kuongeza mwamko:waambie marafiki,jamaa na wafanyakazi wenzako kuhusu umuhimu wa Uvuvi endelevu.
- Usidondoshe takataka, zirejeshe zitumike tena.
- Usijisaidie maeneo ya fukwe. Tumia vyoo vilivyo mbali na vyakula.
- Epuka maradhi hatari kama vile kipindupindu au homa yamatumbo kwa kuokota chaza na makorobwe katika fukwe zilizo safi tu, zilizo mbali na yanapotoka maji machafu.
- Ungana na vikundi vya kijamii kuishawishi serikali iongeze bidii katika kushughulikia takataka na kujenga vyoo vya umma ili kuepusha takataka kutupwa baharini.
- Mwandikie Sheha wako au mbunge ili kumfahamisha kwamba Uvuvi endelevu una umuhimu mkubwa.